BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Nane – Tarehe 16 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

### Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Ripoti ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Ripoti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

149. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Uadilifu, utii na uzalendo ni mambo yanayosaidia kwa kiasi kikubwa katika ukuwaji wa uchumi wa nchi yoyote duniani. Hata hivyo, vitu hivyo vimeendelea kupotea siku hadi siku hapa kwetu Zanzibar.

Je, ni upi mpango wa Serikali katika kunusuru hali hiyo.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

132. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa baadhi ya makosa yanayoibuliwa katika kaguzi mbali mbali za fedha yanatokana na uwezo mdogo kwa wahasibu, na kwa kuwa inaaminika kuwa changamoto hiyo imekuwa ikijitokeza baada ya wahasibu hao kushindwa kukabiliana na mabadiliko ya mfumo wa ufungaji wa hesabu.

Je, ni upi mpango wa Serikali katika kukabiliana na jambo hilo.

### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

44. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kuna baadhi ya njia za ndani ni viunganishi vizuri baina ya barabara kuu kama ilivyo kwa barabara ya Mombasa “round about” – Fumba. Barabara hii pamoja na zinazotegemewa kujengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikiwa ni pamoja na Kisauni – Shakani – Nyamanzi – Fumba, ni viunganishi muhimu sana kwa matumizi ya kiuchumi na kijamii, bila ya kusahau njia ya Shakani Uwandani hadi njia ya Langoni.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuunganisha njia za aina hiyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

88. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa baadhi ya wateja wa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), wakiilalamikia tozo(gharama) ya huduma ya umeme wanayotozwa, wakati wameshailipia kwenye mita na hasa ikizingatiwa kuwa, huduma ya umeme ni sawa na nishati nyengine kama petroli. Vile vile wateja hao wamekuwa wakilalamika kwamba, wafanyakazi wa ZECO wanafanyiwa upendeleo bila ya haki kwa kutolipa tozo/gharama ya huduma *(Service Charge)*.

Je, ni upi msimamo wa Serikali kuhusu kadhia hii na mpango wa kuiondoa gharama hii kwa wateja.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

83. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Suala la kupunguza vifo vya mama na mtoto (Reduction of mother and child mortality rate) ni kauli mbiu ya ulimwengu mzima, kiasi ambacho Zanzibar kwa kuwa nayo ni sehemu ya ulimwengu haiwezi kujitenga nayo. Na hasa ikizingatiwa kuwa katika baadhi ya familia za Kizanzibari, akina mama hujifungua watoto mapacha kuanzia wawili, watatu na zaidi ya hapo, lakini familia hizo zikiwa na uwezo mdogo wa kuwahudumia mapacha hao si kwa maziwa, chakula wala matibabu. Jambo hili linapelekea kudhoofika sana kiafya pamoja na kimaisha kwa watoto hao pamoja na mama mzazi.

(a) Je, ni upi mpango wa sasa wa Serikali wa kuzisaidia familia za mapacha ikiwemo kuwapatia posho la kila mwezi sambamba na kuzipatia familia hizo bima za afya.

(b) Je Serikali ina mipango gani ya kuyanusuru maisha pamoja na kuimarisha afya za mapacha wa aina hii pamoja na mama zao.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

90. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kumekuwa na uvamizi uliokithiri wa maeneo ya wazi (Open Spaces) katika visiwa vya Unguja na Pemba kiasi ya kuharibu mandhari nzuri ya miji na kutoa hofu iwapo patatokea majanga, hasa matetemeko ya ardhi, kwa kukosa maeneo yaliyokusudiwa kukimbilia kama ilivyo katika utaratibu wa mipango miji kimataifa.

Je, maeneo mangapi ya wazi Unguja na Pemba yamebadilishwa matumizi yake na kwa utaratibu upi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

86. MHESHIMIWA MOHAMMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana Utamaduni na Michezo:

Naipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar kwa juhudi inazozichukua za kuwa na mpango mzuri wa kuanzisha viwanja vya mpira katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Pamoja na juhudi hizo lakini kwa muda sasa uendelezwaji wa ujenzi wa kiwanja cha Kangani haujafanyika.

Je ni lini Serikali itaendeleza ujenzi katika kiwanja hicho ili kiweze kutumiwa ipasavyo na wana michezo wa fani tofauti.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

53. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kuna baadhi ya mazao, kama vile uwele, mtama, mbaazi, fiwi, kunde na choroko ambayo hapo zamani yalikuwa yakipatikana sana katika visiwa vya Unguja na Pemba. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, siku hizi uzalishaji wake umekuwa mdogo sana.

Je, ni lini Wizara ya Kilimo itazalisha mbegu chotara (Hybrid) za mazao haya zitakazoendana na Mabadiliko ya Tabia Nchi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

23. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ina muda mrefu haijaajiri walimu kwa idadi kubwa. Kwa bahati njema hivi karibuni, imeamua kutangaza ajira kwa walimu wa kada na ngazi mbali mbali hapa Zanzibar.

Je, ni ipi nafasi ya upendeleo kwa walimu ambao wametumia muda wao mkubwa kwa kujitolea kufundisha maskulini katika mchakato huu wa ajira.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto:**

Ripoti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Ripoti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**16 Septemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**